# *BARUA #09; USHINDI MKUU KWENYE MAISHA.*

Karibu rafiki yangu mpendwa kwenye barua yetu kwenye mwaka wa mafanikio.

Kwenye barua hii tunakwenda kujifunza kuhusu ushindi mkuu kwenye maisha, ambao tunapaswa kuufanyia kazi na tunapoufikia, hakuna anayeweza kutunyang'anya.

Ukweli ni kwamba, kila kitu tunachohangaika nacho kwenye maisha, kuna hatari ya kukipoteza. Iwe ni biashara tunazoanzisha na kukuza, kazi tulizopata, mali na utajiri tuliojipatia na vingine vingi.

Lakini kuna kitu kimoja ambacho huwezi kukipoteza na wala hakuna anayeweza kukunyang'anya kama ukikielewa na kukisimamia vizuri.

Uzuri wa kitu hicho ni kwamba, hakuna anayeweza kushindana na wewe akakushinda,

hivyo ukiwa juu ni juu kweli kweli bila ya kuhofia kupitwa na yeyote.

Kitu ninachokushirikisha leo, tayari unakijua, lakini leo tunakwenda kukichimba kwa ndani zaidi, ili tuondoke na mkakati wa kwenda kufanyia kazi kwenye kila siku ya maisha yetu na kuwa bora.

## Ushindi ulio mkuu.

*Kuwa wewe kwenye dunia inayokazana kukubadilisha uwe kama wengine ni mafanikio makubwa. - Ralph Waldo Emerson*

Mwandishi na mwanafalsafa Emerson aliliweka hilo vizuri kama ilivyo kwenye nukuu yake hapo juu. Kwamba ushindi ulio mkuu kwenye maisha yako, ni kuweza kuwa wewe kwenye dunia ambayo inakazana kukubadilisha uwe kama wengine, uwe vile usivyo wewe.

Tangu umezaliwa mpaka umekua, jamii imekuwa inafanya kazi moja kubwa, kukulazimisha uwe vile inavyotaka yenyewe na siyo vile unavyotaka wewe.

Ulizaliwa ukiwa unajua vitu vichache sana, vya kukusaidia kuishi, ikiwepo kutafuta chakula (kunyonya) na kuepuka hatari. Lakini mengine yote ambayo umejifunza, ni jamii imekufundisha.

Fikiria malezi ambayo umekuwa unayapata tangu mtoto, imani uliyokuzwa nayo, elimu uliyoipata na maisha uliyoaminishwa ndiyo sahihi kuyaishi, yote hayo ni zao la jamii.

Jamii inaweza kuwa ilifanya kwa nia njema kabisa, lakini ni kwa sababu yenyewe haikujua kwamba inakuzuia usiwe na mafanikio makubwa kwenye maisha yako.

Wapo watu ambao walionesha vipaji vizuri wakati wanakua, lakini jamii haikuona thamani ya vipaji hivyo, na wakakatishwa tamaa kuhangaika navyo, badala yake jamii ikawaonesha kipi wanapaswa kufanya.

Kinachotokea ni leo tuna watu wengi ambao wanaishi maisha ambayo hawayafurahii na wanaona hakuna wanachoweza kufanya maana tangu utotoni wameaminishwa jamii iko sahihi.

Fikiria kipindi ukiwa mtoto, hukuwa na njia ya kutimiza mahitaji yako, kuanzia kwenye chakula, usalama na mengine. Yote ulitegemea kwa wazazi na jamii. Hivyo kukiuka kile wazazi na jamii inakuambia, ilikuwa ni hatari ya kukosa yale muhimu na maisha yako kuathirika.

Hivyo kwa asili, tumejifunza kuwa watiifu kwa wale wanaotupa kile tunachotegemea, kuamini wao wako sahihi na tunapaswa kuwasikiliza hata pale wanapokwenda kinyume na kile tunachotaka sisi.

Unaweza kufikiri hali hiyo ingeishia utotoni, lakini tunakuwa tumekariri kiasi kwamba tunaendeleza mpaka tunapokuwa watu wazima na tunaojitegemea.

Kinachobadilika ni mamlaka, ulipokuwa mtoto wazazi ndiyo walikuwa kila kitu kwako. Sasa umekuwa mtu mzima unayejitegemea, lakini mwajiri au serikali imekuwa mamlaka kwako.

Kwa kuwa mwajiri unamtegemea sana kwenye kuingiza kipato cha kuendesha maisha yako, unajikuta unamsikiliza zaidi kuliko

unavyojisikiliza wewe. Kadhalika kwenye serikali, kwa kuwa ina mamlaka makubwa, unaamini iko sahihi zaidi.

Lakini hayo yote siyo sahihi, hasa kwa sasa ambapo umeshakuwa mtu mzima, unayejua kila kitu kina gharama yake, unapaswa kujisikiliza wewe zaidi kuliko unavyowasikiliza wengine.

Kwa kipindi kirefu kwenye maisha yako umekuwa unawasikiliza wengine, na umefika hapo ulipo sasa. Kama unataka kwenda mbali ya hapo ulipo sasa, ni wakati wa kujisikiliza wewe mwenyewe.

Kwa sababu wewe ndiye unayejijua vizuri kuliko mtu mwingine anavyoweza kukujua.

Kwa sababu wewe ndiye mwenye ajenda yenye manufaa kwako, wengine wote wanaokutaka uwasikilize na kufanya wanachotaka, ni kwa sababu wana ajenda zao binafsi, wana maslahi yao na wanakuhitaji katika kuyakamilisha.

Hakuna ubaya kwenye kuwasaidia wengine kuyakamilisha maslahi yao, lakini unapaswa kufanya hivyo ukijua kabisa na siyo kwa kuhadaiwa kwamba unafanya kwa kuwa ni kitu muhimu kwako.

Kuwa wewe, kwenye dunia ya aina hii, dunia ambayo inapambana usiku na mchana ili usiwe wewe, ni ushindi mkubwa sana.

## Asilimia 99 na asilimia 1.

Baada ya anguko la uchumi la mwaka 2008, nchi ya marekani ambayo ndiyo iliathiriwa sana, kuliibuka maandamano makubwa kwenye mtaa maarufu kwa shughuli za kifedha na uwekezaji dunia unaoitwa Wall Street.

Mtaa huo ndiyo kiini cha ubepari duniani, mabenki makubwa na masoko ya hisa yakiwa yanaendeshwa hapo. Kwa kuwa anguko hilo la kiuchumi ni moja ya madhaifu ya mfumo wa ubepari, wananchi wa kawaida waliona mfumo huo unawaumiza.

Katika anguko hilo, walioathirika zaidi ni tabaka la chini na la kati. Lile tabaka la juu kabisa halikuonekana kuathirika. Na hapo ndipo makundi mawili yalipotengenezwa, asilimia 1 ambayo ilinufaika sana na kutokuumia na asilimia 99 ya walioumia.

Walioandamana walijinadi wazi kwamba wako kwenye asilimia 99, kundi la walioumizwa na anguko hilo.

Kwenye kila jamii, makundi ya aina hii yanajitokeza wazi kabisa, kuna wengi ambao wana maisha ya chini au ya kawaida, halafu kuna wachache sana ambao wana maisha ya juu au wana mafanikio makubwa.

Kila jamii huwa haiwaelewi watu hao, kwa sababu maisha yao huwa ni ya tofauti kabisa na ya walio wengi. Hivyo kwenye kila jamii, kulingana na kiwango cha ustaarabu, watu hao hupewa majina mbalimbali.

Kwa mataifa yaliyoendelea, watu hao wataitwa wanyonyaji na wenye nguvu ya kushawishi

tawala ziwanufaishe wao na kuwaumiza wengine.

Kwenye nchi zinazoendelea hadithi huwa ni tofauti. Pata picha ya jamii ilivyokuwa inawaita wale waliofanikiwa kabla hujajua kuhusu mafanikio. Kwenye jamii zetu, wale waliokuwa wamepiga hatua zaidi walipewa kila aina ya majina, waliitwa wachawi, wenye majini, freemason na mengine ya aina hiyo.

Nakumbuka wakati nakua kijijini, tajiri yeyote ambaye mzazi au mtoto wake alikufa basi ilisemekana amemtoa kafara. Kwa wale ambao walipata watoto wenye ulemavu fulani, ilisemekana wamewageuza watoto hao kuwa mandondocha na kuwatumia kama sehemu ya kupata utajiri.

Kitu ambacho hadithi hizo zinakosa ni kushindwa kueleza kwa nini mambo kama hayo yanatokea kwa wale ambao hawajafanikiwa pia. Ambao hawajafanikiwa wanafiwa na wazazi au watoto wao, wanapata watoto ambao wana

ulemavu, lakini hutazisikia hadithi za kwamba hizo ni kafara za kupata mali.

Kwa kuangalia aina ya hadithi ambazo jamii imekuwa inajipa katika kuwatofautisha wachache wanaofanikiwa sana na wengi wanaoishia kuwa kawaida, tunajifunza kitu kimoja, jamii haiwaelewi wale wachache wanaofanikiwa sana.

Na sisi binadamu huwa hatuwezi kuvumilia kitu ambacho hatukielewi, badala yake tunatengeneza hadithi inayoendana na kile tunachotaka kuamini.

Ukweli ni kwamba, wale wachache sana wanaofanikiwa, ni wale ambao wamepata ushindi mkuu kwenye maisha yao, wamechagua kuwa wao kwenye jamii inayowalazimisha wawe kama wengine.

Hiyo ndiyo maana jamii haiwaelewi na hata hadithi ambazo jamii inajipa kuhusu watu hao, ni kwenye matukio ambayo watu hao wanayafanya tofauti na jamii ilivyozoea.

Chukua mfano wa wafanyabiashara wa baadhi ya makabila ambao huwa wanaonekana ni wabahili sana, ambao wanaweza hata kuanguka kwa njaa wakiwa na fedha mfukoni, wasithubutu kutumia fedha hiyo kwa chakula kwa sababu hilo siyo lengo.

Ukiangalia maisha ya wafanyabiashara hao, ni ya tofauti kabisa na ya jamii inayowazunguka. Wao wanakuwa wameweka kipaumbele kikubwa kwenye biashara wanazofanya na mengine wanaachana nayo. Wanakuwa wamejijengea nidhamu ya hali ya juu mno. Vitu hivyo, vinawatofautisha kabisa na jamii na ndiyo vinawaletea mafanikio makubwa.

Sasa jamii kwa kuwa haielewi tofauti yao, inakuja na hadithi, wanafanya hivyo kwa sababu ndiyo masharti waliyopewa na waganga au majini waliyopewa. Lakini hizo zote ni hadithi za wale wasioujua ukweli.

Wakati mwingine hata hao waliofanikiwa hawaijui sababu, kama ambavyo samaki hajui kama yuko kwenye maji, wao inakuwa ni

sehemu ya maisha yao kuwa hivyo, lakini kwenye jamii ni kitu cha tofauti.

Sisi tuna bahati ya kujua sayansi iliyo nyuma ya mafanikio makubwa ya baadhi ya watu ambao jamii haiwaelewi, na hivyo tuna fursa ya kufanya hivyo kwa ubora na kufanikiwa zaidi.

Kwa kujua kwamba wale wanaofanikiwa sana, kwenye kila eneo la maisha ni wale ambao wamepata ushindi mkuu, wa kuweza kuwa wao kwenye jamii inayowalazimisha wawe wasivyokuwa, tunapata njia sahihi ya sisi kufikia mafanikio makubwa pia.

Hivyo hatua ya kwanza na ya msingi kabisa kama bado hujaipiga kwenye maisha yako, ni kuchagua kuwa wewe na kutokukubali kwa namna yoyote ile jamii ikubadilishe na kuwa kitu kingine.

## Unawezaje kuwa wewe?

Kuwa wewe ni hatua ya kwanza na ya muhimu kwako kuwa na mafanikio makubwa kwenye maisha. Lakini je unawezaje kuwa wewe?

Ukienda dukani kununua simu mpya, unapewa simu ikiwa kwenye boksi na ndani ya boksi hilo kunakuwa na vifaa vyote vya simu, pamoja na kijitabu kinachoelezea jinsi ya kutumia simu hiyo.

Hivyo ndivyo unavyoweza kuijua simu na jinsi ya kuitumia. Kama kuna mahali umekwama wakati wa kutumia simu, unarudi kwenye kijitabu na kusoma maelekezo sahihi.

Hivyo ndivyo ilivyo kwa kila kifaa kinachotengenezwa na binadamu, kinaambatanishwa na kijitabu cha maelekezo ya kukitumia (user's manual).

Lakini kwenye maisha yetu sisi binadamu, mambo ni tofauti, ulipozaliwa, ulikuja ukiwa mpya kabisa hapa duniani, lakini ujio wako haukuambatana na kijitabu kinachokuelezea wewe.

Hivyo tangu utoto wako, hakuna ambaye amewahi kukujua wewe kwa undani. Badala yake watu wamekuwa wanabahatisha tu. Kadiri unavyokua ubashiri wa watu unazidi kubadilika.

Bila shaka katika kipindi cha ukuaji wako umewahi kutabiriwa mambo mbalimbali, labda nyumbani walikuona unapenda kuhoji sana maswali na wakakuambia utakuja kuwa mwanasheria. Shuleni walikuona ukiwa na dadisi sana na kukuambia utakuja kuwa mwanasayansi. Marafiki zako walikuona ukipenda sana muziki na kukuambia utakuja kuwa msanii.

Ulitabiriwa mengi, na wewe mwenyewe ulijitabiria mengi na ya tofauti, ambayo kwa sehemu kubwa hujawa kwenye maisha yako. Yote hiyo ni kwa sababu hakuna anayekujua kwa undani.

Na kwa bahati mbaya zaidi, kwa namna jamii imekutengeneza, imekunyima kabisa hata nafasi ya kujijua wewe mwenyewe. Imekusisitiza na kukuaminisha kwamba unachopaswa kuwa ni vile jamii ilivyokuandaa kuwa na tofauti na hapo utapotea.

Ndivyo tunavyopata watu wazima, ambao hawajitambui wao wenyewe, wakiendesha

maisha yao kwa mkumbo na kutokuyafurahia licha ya hatua wanazokuwa wamepiga.

Hatua muhimu kabisa ya kuwa wewe ni KUJITAMBUA.

Kujitambua wewe mwenyewe, ndiyo msingi mkuu wa falsafa nyingi duniani.

Mafunzo yote ya maendeleo binafsi yanaanzia kwenye mtu kujitambua yeye mwenyewe.

Ni kupitia mtu kujitambua ndiyo anaweza kuwa yeye na kufanya makubwa kwenye maisha yake.

Hata tukiangalia maisha ya walimu na wanafalsafa wakubwa ambao waliibadili duniani, mwanzo walikuwa ni watu wa kawaida tu. Lakini wakapitia kwenye mazingira yaliyowalazimisha kujitambua na kuanzia hapo wakawa wao na kufanya makubwa.

Maisha yako yanabadilika kabisa pale unapojitambua wewe mwenyewe na hapo ndipo mafanikio makubwa, ambayo hayawezi kuangushwa na yeyote yanapozaliwa.

Katika kujitambua wewe mwenyewe, kuna maswali matatu unayopaswa kuyajibu ambayo majibu yake ndiyo yanakuwa mwongozo wa maisha yako.

Maswali hayo matatu yamekuwa ndiyo msingi wa dini na falsafa nyingi, lakini yamekuwa yakijibiwa kwa kundi zima badala ya mtu mmoja mmoja kuyajibu na kuyaishi kwenye maisha yake.

Swali la kwanza ni wewe ni nani?

Unapojiita mimi, huyo mimi ni nani? Kwa sababu mimi siyo mkono ulionao, maana huwa unasema mkono wangu. Ina maana mkono ni kitu kinachomilikiwa na wewe, je huyo wewe ni nani?

Katika kujibu swali hilo, ndipo tunajifunza kwamba sisi ni roho ambazo zinaishi kwenye miili tuliyonayo. Sisi ni utashi huru tulionao, kwa sababu kila tulichonacho hata mbuzi anacho.

Kwa kujua hilo, kwamba wewe ni utashi huru, unaoweza kufikiri na kufanya maamuzi, ni ushindi mkubwa mno kwenye maisha yako. Wengi wanayaishi maisha yao bila kutambua hilo. Wengi hawajawahi kufanya maamuzi yoyote makubwa kwenye maisha yao, badala yake wanafuata tu mkumbo.

Wewe ni utashi huru, unaoweza kufikiri na kufanya maamuzi ni jibu la kwanza katika kujitambua wewe mwenyewe.

Swali la pili ni nini kusudi la wewe kuwa hapa duniani?

Swali hili limekuwa linaibua mijadala ya kila aina. Wapo wanaoamini maisha yetu hapa duniani ni kama ajali, tumekuja na tutapita na dunia itaendelea kuwepo. Hawa wanaamini maisha yetu hayana tofauti na ya mnyoo. Lakini wale wanaofikiri hivyo, wanajipa upofu wa namna dunia inavyobadilishwa na watu wachache. Ukiangalia historia ya dunia, tangu mwaka 1900 mpaka mwaka 2000, matukio makubwa kabisa ya kihistoria na yaliyoibadili

dunia, yalisababishwa na watu wasiozidi 10. Lenin, Hitler, Mussolin, Churchill, Mao na Stalin ni baadhi ya wale waliochangia kwenye matukio makubwa kabisa ya karne ya 20.

Hata tukiangalia karne tuliyopo sasa, kwa miaka 20 iliyopita, kuanzia 2000 mpaka 2020 tunaona matukio makubwa na maendeleo makubwa kabisa kwenye sayansi na teknolojia yamechochewa na watu wachache. Tukichukua mfano wa Steve Jobs, ugunduzi wake wa simu janja, umekuwa na athari kubwa mno kwenye dunia ya sasa.

Hivyo ni dhahiri bila ya shaka yoyote kwamba maisha yetu yana kusudi na wachache wanaobahatika kujua kusudi hilo ndiyo wamekuwa wanaleta mabadiliko makubwa hapa duniani. Kama tunaona maisha hayana kusudi, ni kwa sababu tunawaangalia wengi ambao wanapita hapa duniani kimya kimya.

Lakini tukirudi kwenye kanuni ya asilimia 99 na asilimia 1 tunaona kwa nini wachache ndiyo

wanaonekana kuwa na maisha ya kusudi huku wengine wakipita hapa duniani kama minyoo.

Ubaya wa kusudi ni kwamba hakuna anayeweza kukuambia, kwa kuwa hakuna anayejua kipi kilicho ndani yako. Na wewe mwenyewe ni vigumu kujua kwa sababu umeshahadaiwa sana maisha yako yote kiasi kwamba umejipuuza kabisa.

Lakini uzuri ni kwamba, kuna nafsi fulani huwa ipo ndani ya kila mmoja wetu, nafsi ambayo ni halisi kwa mtu na huwa haifi. Hata mtu ajisahau kiasi gani, hata abadilishwe kiasi gani, kuna nafsi ambayo huwa haifi.

Hii ndiyo nafsi iliyobeba kusudi la mtu hapa duniani.

Ili kuweza kulijua kusudi lako, unapaswa kuisikiliza nafsi hiyo, kuipa uhai na nafasi, kuisikiliza na kuchukua hatua kwenye yale unayojifunza kuhusu wewe binafsi.

Kwa mfano kila mtu kuna kitu ambacho anapendelea kufanya au kufuatilia kuliko vitu

vingine vyovyote. Kuna vitu mtu yuko tayari kuacha kula lakini asivikose. Kuna vitu mtu atafanya hata kama hakuna anayeangalia au anayemlipa. Vitu hivi anavifanya kwa sababu vinatoka ndani yake na siyo kwa sababu anataka kuwaridhisha wengine.

Moja ya matokeo ambayo jamii imepata katika kutufanya tusiwe halisi ni kuhakikisha tunafanya vitu kuwafurahisha wengine na siyo sisi wenyewe. Lakini ile nafsi ya ndani yako ambayo haifi, bado hukusukuma ufanye vile vilivyo halisi kwako bila kujali wengine wanakuchukuliaje.

Kusudi la maisha yako ni swali ambalo hakuna anayeweza kukujibia, hata kama angekuwa na nia njema kiasi gani, hakuna mwenye uwezo huo.

Pia ni swali ambalo kwako binafsi ni gumu kulijibu kwa sababu umeshadanganywa na kuhadaiwa sana. Lakini unapochagua kujisikiliza tena, unapokuwa tayari kujaribu mambo

mbalimbali, unakutana na kile kinachoifufua nafsi yako na hilo ndiyo kusudi lako.

Swali la tatu ni maisha yako yana maana gani?

Swali la pili ambalo ni la kusudi linakuhusu wewe binafsi, swali la tatu kuhusu maana ya maisha yako linawahusu wengine, jinsi ambavyo maisha yako yanagusa maisha ya wengine.

Kwa mifano niliyokushirikisha kwenye swali la pili, tumeona jinsi historia imejengwa na watu wachache, lakini wapo walioijenga kwa namna chanya na yenye manufaa kwa wengine na wapo waliojienga kwa namna hasi na iliyokuwa na madhara makubwa kwa wengine.

Tukirudi tena kwenye historia ya wale waliofanya yenye madhara kwa wengine, tunaona wazi kwamba mwanzoni walikuwa na nia njema, lakini kwa kutokujua madhara ya kile wanachofanya, wakaishia kuleta uharibifu mkubwa. Hawakuweza kuona udhaifu wao na hilo ndiyo lilipelekea uharibifu waliosababisha.

Ili kuepuka kuingia upande wa wale wanaofanya uharibifu, lazima ujue maana ya maisha yako, kwa kuwa wewe, kwa kujua kusudi lako na kuliishi, wengine wananufaikaje?

Hili ni swali ambao wengi wamekuwa hawajiulizi na kujijibu, na ndiyo sababu kwenye zama tunazoishi sasa, pamoja na maendeleo makubwa ya kiteknolojia, maisha ya wengi yako hivyo.

Kwenye zama tunazoishi sasa, dini na hata jamii zimepoteza nguvu ambayo vilikuwa nazo kipindi cha nyuma. Mfano zamani dini zilikuwa na mamlaka ya kuwapangia namna ya kuishi maisha yao na watu walitii kwa sababu hakukuwa na mbadala. Kadhalika jamii ziliwapangia watu jinsi ya kuishi, kazi gani wafanye, waoe au kuolewa na nani na watu walitii.

Kwa sababu taasisi hizo zilikuwa na nguvu ya kuwatawala watu, hazikuona umuhimu wa kuwafundisha watu kuwa wao. Sasa taasisi hizo zinakosa nguvu na watu hawajui jinsi ya

kuamua mambo yao wenyewe na hivyo kujikuta wakifuata tu mkumbo.

Kwa kujitambua wewe mwenyewe, unaondoka kwenye mkumbo, unaacha kufanya mambo yasiyokuwa na maana kwako na yasiyo na manufaa kwa wengine.

Ni pale unapoweza kuishi kwa viwango vya aina hiyo, pale unapokuwa na majibu ya maswali hayo matatu na kuyaendesha maisha yako kulingana na maswali hayo, ndiyo unakuwa umefikia ushindi mkubwa kwenye maisha, ushindi ambao hakuna anayeweza kukunyang'anya.

Unakuwa wewe kwa kujua wewe ni nani, una kusudi gani na maisha yako yana maana gani. Nje ya hapo, bado hujawa wewe, badala yake ni kipande kidogo kwenye jamii kubwa ambayo inajiendea tu kwa mazoea.

## Madhaifu na uimara wako.

Katika kujitambua, pamoja na kuyajibu maswali muhimu matatu, kuna vitu hivi viwili

unavyopaswa kuvijua kuhusu wewe. Vitu hivyo ni uimara na madhaifu yako.

Kila mtu ana uimara, kuna vitu ambavyo unaweza kuvifanya kwa ubora kabisa kuliko wengine wanavyoweza kufanya. Lakini pia una madhaifu, kuna vitu huwezi kuvifanya vizuri.

Sasa jamii kwa kutaka kukutawala, huwa inafanya hivi, inakuambia ufiche uimara wako kwa sababu kuuonesha itakuwa ni kiburi. Halafu inakuambia ukazane kuondoa udhaifu wako ili usiwe kikwazo kwako.

Kwa kufanya hayo mawili, unajikuta unadumaza uimara wako, huku ukiimarisha udhaifu wako.

Unachopaswa kufanya ni kutambua uimara wako na kuutumia vizuri. Tambua kile ambacho uko vizuri kwenye kukifanya kuliko wengine na hicho ndiyo kiwe msingi mkuu wa kazi au biashara yako.

Halafu kwenye madhaifu yako, usiyafiche na wala usijaribu kuyarekebisha, badala yake yakubali na angalia namna ambavyo utayazuia

yasiwe kikwazo kwako. Mfano kama kuna kitu muhimu unapaswa kufanya lakini kipo kwenye madhaifu yako, tafuta mtu mwenye uimara kwenye hilo kisha shirikiana naye.

Kujaribu kubadili madhaifu yako ili uwe imara ni kupoteza nguvu zako, hivyo unaishia kuwa na madhaifu imara na uimara wako badala ya kuutumia kufanya yaliyo sahihi, unakuwa umeupotezea kwenye kuboresha madhaifu yako.

Usione haya kusema hujui au huwezi, hakuna anayejua au kuweza kila kitu, ila kila mtu anajua na kuweza eneo fulani. Hapo ndipo pa kujenga msingi wako na kushirikiana na wengine kwenye maeneo ambayo wako vizuri.

## Kwa nini ni vigumu kuwa wewe.

*“Man is the only creature who refuses to be what he is.” — Albert Camus*

Kauli ya mwanafalsafa Albert Camus imejibu vizuri kabisa swali hilo la kwa nini ni vigumu kuwa wewe.

Turudi kwenye asili, kama una shamba na umepanda mchungwa na mlimao karibu karibu, mwisho wa siku mchungwa utakuwa mchungwa na kuzaa machungwa, huku mlimao utakuwa mlimao na kuzaa malimao.

Kadhalika kama unafuga, ukaweka kuku na kanga kwenye banda moja, ukawapa chakula kimoja, bado kuku atabaki kuwa kuku na kanga atabaki kuwa kanga.

Maajabu sasa, waweke watu wawili kwenye eneo moja, iwe ni kazi au biashara na baadaye unakuja kukuta wote wanafanya vitu vinavyofanana.

Camus aliona mbali aliposema binadamu ndiye kiumbe pekee ambaye anakataa vile alivyo.

Na sababu tunayo, tumeshajifunza hapo juu, tangu tukiwa wadogo tumekuwa tunaitegemea sana jamii, hivyo tumejifunza na kuamini kwamba, wengine, hasa wanapokuwa wengi wapo sahihi kuliko sisi.

Ni vigumu kuwa wewe kwa sababu jamii imekuhadaa kuwa kama inavyotaka wewe. Imekutega uingie kwenye mashindano na wengine, mashindano ambayo hata ukishinda, hakuna unachonufaika nacho zaidi ya jamii kuwa imepata inachotaka.

Hivyo mapambano yetu makubwa katika kupata ushindi mkuu, katika kuwa sisi, ni kushinda nguvu hii inayotusukuma tuwe tofauti na uhalisia wetu.

Nguvu hii huwa hatuielewi kwa sababu ukishakuwa mtu mzima, haitoki tena nje, bali inakuwa imeshapandikizwa ndani yako.

Unaona watu wanafanya kitu fulani, ghafla na wewe unataka ukifanye, siyo kwa sababu ni kitu kinachotoka ndani yako, bali ni udhaifu ambao umeshajengewa.

Na kama nilivyokuambia, udhaifu huu huwa unainufaisha jamii na wengine kuliko unavyokunufaisha wewe.

Chukua mfano mdogo wa fursa za kitapeli ambazo huwa zinakuja kila siku na kupelekea watu kupoteza fedha na muda wao. Fursa zote hizo zinafanikiwa kwa sababu ya udhaifu ambao upo ndani yetu, udhaifu wa kukataa kuwa sisi.

Kila fursa ya kitapeli inayokuja, huwa inaonesha vitu viwili, moja kuna wenzako ambao wanapata manufaa makubwa ambayo wewe huyapati. Na mbili kama hutachukua hatua sasa utakosa huku wenzako wakiendelea kunufaika.

Utapewa mifano ya wale walionufaika na fursa hiyo, ambayo mingi siyo ya kweli. Utapewa shuhuda za wale walionufaika, ambazo siyo za kweli. Yote hiyo ni kuhakikisha unajisahau wewe na kuanza kujilinganisha na wengine, kujipima nao na kuona wewe umeachwa nyuma.

Inapoongezeka hali ya uharaka, kwamba kama hutachukua hatua sasa basi utakosa, unakimbilia kuchukua hatua na unaishia kuliwa. Kama umewahi kudanganywa kwa namna hiyo, ukikaa chini na kutafakari unagundua wazi

kwamba hukuwa unajifikiria wewe wakati unachukua hatua. Na hata kama ulikuwa unajifikiria, siyo kwa kujiangalia wewe mwenyewe, bali kwa kuangalia wengine wanavyonufaika huku wewe ukiachwa nyuma.

Ukijitambua na kuwa wewe, hakuna anayeweza kukutapeli au kukuibia, kwa sababu hujaribu kubadilika na kuwa usichokuwa, huumizwi na wengine kunufaika kuliko wewe, kwa sababu unajua wao siyo wewe na wewe siyo wao.

## Ushawishi mdogo mdogo unaoendelea kwenye maisha yako.

Unaweza kuwa umejifunza haya ninayokushirikisha hapa, lakini ukajiambia wewe ulishaacha kuisikiliza jamii zamani.

Labda ukaenda mbele na kujiambia kwamba ulishaachana na mila zisizokuwa na maana kwako, au ulishabadili dini kutoka ile ambayo ulilelewa na kukua nayo hivyo umeamua mwenyewe.

Wengine wanaweza kusema wamejenga mfumo tofauti kabisa wa imani na kuamua kuachana na dini, kwa sababu zimekuwa kikwazo kikubwa kwa wengi. Na hapo mtu ataamini yuko huru, anafanya maamuzi yake mwenyewe na siyo kushinikizwa na yeyote.

Nina habari zisizo nzuri sana kwako, haupo huru kama unavyodhani upo. Kwani kuna ushawishi mdogo mdogo ambao umekuwa unaendelea kwenye maisha yako bila ya wewe kujua.

Kuna nguvu kubwa inayoendelea kukushawishi na kuchochea au kuzuia baadhi ya maamuzi yako, lakini hujui kuhusu nguvu hiyo na jinsi inavyofanya kazi.

Nguvu hiyo ni propaganda, jumbe mbalimbali unazolishwa kila siku, zenye lengo la kupandikiza imani fulani ndani yako ili ufanye maamuzi fulani.

Unaweza kushangaa kuhusu propaganda, ukijiambia kwa sasa hakuna propaganda kwa sababu hakuna vita au hali kama hizo zinazochochea uwepo wa propaganda.

Lakini nikuambie kitu kimoja, propaganda hazijawahi kukoma kwenye jamii ya binadamu. Na kuna propaganda za aina tatu, zinazoendeshwa na utawala, zinazoendeshwa na biashara na zinazoendeshwa na kundi la watu.

Tangu enzi na enzi, kumekuwa na njia ya kusambaa kwa propaganda, lakini karne tunayoishi sasa, imekuwa rahisi zaidi na ushawishi wake ni mkubwa. Kipindi cha nyuma vyombo vya habari vilitumika kusambaza propaganda na hivyo zililenga watu wengi kwa wakati mmoja.

Lakini kwa zama hizi, propaganda zinasambazwa kwa mitandao ya kijamii na hatari ya mitandao hiyo ni kwamba inakujua wewe kuliko unavyojijua mwenyewe. Imekusanya taarifa zako nyingi na kuzitumia kukuletea vitu vinavyoendana na wewe, kitu kinachokuwa rahisi kushawishika.

Kila habari unayoiona, kila tangazo unalokutana nalo, ni sehemu ya propaganda mbalimbali.

Umewahi kujiuliza kwa nini matangazo ya vilevi au starehe mbalimbali huwa yanatumia watu wenye sura na mwonekano mzuri? Unajua kabisa kila kilevi kinachosha mwili na mtu akilewa anakuwa hovyo, lakini huwezi kuliona hilo kwenye matangazo yanakushawishi utumie kilevi hicho.

Hiyo ni kwa sababu matangazo hayo ni propaganda, taarifa zinazokutaka uamini kitu ambacho siyo. Unaaminishwa ukitumia kilevi hicho utakuwa na mwonekano mzuri kama wale unaowaona kwenye tangazo husika.

Sasa nguvu ya propaganda haipo kwenye ujumbe unaotolewa, bali ipo kwenye kurudiwa rudiwa kwa ujumbe huo. Unapoona habari au tangazo usilokubaliana nalo kwa mara ya kwanza, unaweza kubisha na kukataa. Lakini pale tangazo au habari hiyo inapokujua kila siku na kwa namna tofauti, akili yako inaanza kupokea na kukubali kwamba ni kitu sahihi.

Hivyo ndivyo propaganda mbalimbali zinavyofanya kazi kwenye maisha yako, na

ndiyo nguvu kubwa ya ushawishi inayotumika kukusukuma wewe ufanye maamuzi fulani bila ya kujua umeshinikizwa.

Kama unatumia mitandao ya kijamii, unafuatilia habari na hata tamthilia mbalimbali, jua kuna ujumbe unaokuwa nyuma ya vitu hivyo, ambao lengo lake ni kukushawishi wewe ukubali au kufanya vitu fulani.

Na tukirudi kwenye udhaifu wetu tuliojifunza, udhaifu wa kukiamini kundi kuliko tunavyojiamini binafsi, propaganda huwa zinatengenezwa kutuonesha kwamba wengine wote wanakubaliana na kitu fulani isipokuwa sisi tu.

Kwa kila maamuzi unayofanya kwenye maisha yako, tambua nguvu ya propaganda mbalimbali zinazoendeshwa kukushawishi.

Katika kuchagua kujitambua, kuwa wewe na kuyaishi maisha yako, tambua nguvu ya propaganda inayoweza kutumiwa kukulaghai uone unakuwa wewe kumbe unakuwa vile

unavyotaka kumbe unakuwa namna wengine wanataka uwe.

Kuwa makini na kila kinachoingia kwenye akili yako, kupitia kuangalia, kusikiliza na hata kusoma. Hata vitabu unavyosoma, vingi vina ajenda ambazo haziko wazi, vikiwa na lengo la kufanya uone vitu fulani ni kawaida na kukubaliana navyo.

Hoji kila kitu, dadisi, chochote unachokubaliana nacho au kuamini, hakikisha una ushahidi wa kufanya hivyo. Hiyo ndiyo njia pekee ya kushinda nguvu ya propaganda, ambayo kwa zama hizi za mitandao ya kijamii, imewateka wengi.

## Ni vita isiyo na mwisho.

*To be nobody-but-yourself-in a world which is doing its best, night and day, to make you everybody but yourself-means to fight the hardest battle which any human being can fight, and never stop fighting. - E.E. Cummings*

Kama unafikiri ukishajitambua na kuyaishi maisha yako ndiyo umemaliza vita, umefika kwenye usafi ambao huwezi kuchafuka tena, unajidanganya.

Kuwa wewe ni vita isiyo na mwisho, vita utakayopambana nayo maisha yako yote kwa sababu wale wanaotaka usiwe wewe hawachoki na kila wakati wanakuja kwa namna tofauti.

Ukishinda kundi moja linakuja kundi jingine, ukivuka propaganda moja inakuja nyingine, ukishinda wakati mmoja, kuna mwingine unakuja. Ni vita mwanzo mwisho, sawa na kuogelea kwenye kina kirefu ambapo huoni ukingo, ambapo lengo lako kuu ni kuhakikisha kichwa kinakuwa juu ya maji.

Wengi wa wanaopambana na wewe kwenye vita hii, hawajajitambua wenyewe, hivyo hawakuoni wewe kama shujaa, badala yake wanakuona kama msaliti, ambaye umewatenga wenzako.

Hivyo watapambana sana, watatumia kila mbinu kukuangusha, kwa sababu wanaamini wanafanya kilicho sahihi. Watatafuta kila udhaifu wako na kuhakikisha wanautumia kukurudisha nyuma.

Hivyo kamwe usijisahau, usijione umepata ushindi wa kudumu, ndiyo ni ushindi mkubwa, lakini lazima uendelee kuulinda.

Moja ya silaha ambazo wale wanaotaka kukuangusha kwenye ushindi wako wanazitumia ni silaha ya hatia. Silaha hii imekuwa inatumika tangu enzi na enzi na imekuwa inawaangusha sana wale ambao ni dhaifu, ambao hawajaweza kuyajibu maswali matatu tuliyojifunza hapo juu.

Chukua mfano wa matajiri au wale waliofanikiwa sana. Mara nyingi hawa ni watu ambao wana nidhamu ya hali ya juu mno kwenye yale wanayofanya. Kama nilivyoshirikisha kwenye mfano, mtu huyo anaweza kuwa na fedha nyingi, lakini akajinyima vitu anavyovipenda sana. Mtu huyo

anaweza kuwa na ndugu au watoto, wanaoona kwa mali au utajiri alionao, basi anapaswa kuwapa kila wanachotaka. Mtu huyo anapokataa kuwapa wanachotaka, ataonekana mwenye roho mbaya na asiyejali. Maneno mengi juu yake yatasemwa, hadithi nyingi na zisizo za kweli zitaelezwa.

Lakini mtu huyu ndiyo maisha yake, hata kwake mwenyewe anajinyima, lakini jamii haitapenda hivyo, na hapo itapambana naye.

Sasa kama mtu huyu hajafikia kujitambua binafsi kwa hali ya juu, na kujua hata kwa kuwanyima watu kile wanachotaka kuna manufaa makubwa zaidi kwao, atakubaliana nao ili tu asionekane ni mbaya au asiyejali. Na hapo ndipo kila alichojenga kinapobomoka.

Chochote ulichojenga kwa kuwa wewe, kitaanguka vibaya pale utakapoacha kuwa wewe na kushawishika kuwa vile wengine wanavyotaka uwe.

Na hivyo ndivyo wale wanaokuzunguka na jamii wanataka uwe, namna wanavyotaka wao,

pambana kukataa hilo, ni vita utakayopigana maisha yako yote.

## Usumbufu upi unaohangaika nao na kukuzuia kuwa wewe?

Muda tulionao kwenye maisha ni ule ule, kwa waliofanikiwa na ambao hawajafanikiwa. Wote tuna masaa 24 pekee kwenye siku zetu, hakuna mwenye ziada wala hakuna mwenye pungufu.

Lakini katika masaa hayo 24, kuna ambao wanafanya makubwa na kufanikiwa na kuna ambao wanasukuma tu siku ziende. Inakuwaje hapa, nini kinachowatofautisha watu? Mbona kila mtu anaonekana yuko 'bize' na hana muda, lakini matokeo yanayopatikana ni tofauti?

Jibu ni usumbufu, kwa wale ambao hawajajitambua na kuwa wao, jamii imehakikisha ina kitu cha kuwaweka 'bize' ili wasipate nafasi ya kujitambua. Hivyo kwenye jamii kuna usumbufu wa kila aina ambao unaendelea, lengo lake ikiwa ni kuwatinga na

kuwachosha watu ili waendelee kuwa vile walivyo.

Mambo mengi yanayopewa nafasi na umaarufu mkubwa kwenye jamii, ni usumbufu wa kuhakikisha huwi wewe, ni namna ya kukunasa kwenye mambo yasiyo na manufaa kwako ili uwe vile jamii inavyotaka uwe.

Starehe, anasa, makundi, dini, maovu ni njia za kuepuka kuwa wewe.

Mwandishi mmoja amewahi kusema iwapo kila mtu angejitambua na kuishi maisha yake, vilevi vyote vingekosa soko, magereza yangekosa wafungwa, majungu yasingepata nafasi na hata habari zingekuwa hazina maana kabisa.

Hivi unafikiri mtu aliyejitambua, anayejijua yeye ni nani, ana kusudi gani na maisha yake yana maana gani atakaa baa kila siku kulewa? Kwa namna anavyokuwa na mengi yanayomhitaji, hawezi kupata muda wa kupoteza kiasi hicho.

Kila aina ya ushabiki ambao watu wanao kwenye maisha, ni usumbufu unaowazuia

kujitambua na kuwa wao. Fikiria mtu anayejiambia kwamba ni shabiki mkubwa wa mchezo au timu fulani, kwamba ikiwa inacheza lazima atenge muda na kuangalia na hakuna kitakachomzuia kwenye hilo.

Unafikiri mtu huyu amejitambua kweli kweli na kujua moto mkubwa unaowaka ndani yake? Jibu ni hapana, huyu tayari ameshamezwa na propaganda ya michezo ambayo inatangazwa sana na kuamini anaipenda, kumbe ni sehemu ya usumbufu unaomnasa.

Sijui kama unanielewa vizuri hapa kwenye propaganda hata kwenye michezo, wacha twende na mfano. Wewe ni Mtanzania, ambaye unajiambia ni mshabiki kindakindaki wa timu ya mpira wa miguu ya Arsenal ya nchini Uingereza. Hivi unafikiri umekuwa shabiki wa timu hiyo kwa sababu unaipenda sana au inacheza vizuri kuliko nyingine? Kama jibu ni ndiyo basi jua unajidanganya na umenasa kwenye propaganda. Kwanza tambua karibu kila nchi duniani ina ligi ya mpira wa miguu, sasa kwa nini usiwe shabiki wa timu ya nchini Uruguay ila

ukawa shabiki wa timu ya nchini Uingereza? Jibu unalo, propaganda.

Chochote kinachokushawishi ukipende kuliko unavyojipenda binafsi, kuliko ulivyo tayari kuwa wewe na kuishi maisha ambayo ni halisi kwako, ni usumbufu kwako na unaokuwa kikwazo kwako kuwa wewe.

Wakati mwingine usumbufu huo unakupa ushindi hewa, ushindi ambao hauna manufaa ya moja kwa moja kwako. Na hapa tutarudi kwenye mfano wa michezo, maana hiyo ndiyo rahisi na iko wazi, lakini kila eneo lina athari hizo.

Wewe kama shabiki wa timu ya Arsenal, imecheza na Manchester United na timu ya Arsenal ikashinda magoli mawili kwa moja. Siku hiyo unajisikiaje? Unajiambia leo tumeshinda, tumewafunga hao, tunajua zaidi na kadhalika. Sijui unaiona hiyo lugha unayotumia? Unajimilikisha ushindi wa timu iliyo mbali, ambayo haijui hata uwepo wako, lakini ushindi wake unakuwa ushindi wako.

Hii ndiyo aina ya ushindi feki ninaokuambia hapa, usumbufu unakufanya uone umeshinda, lakini ni ushindi feki, kwani maisha yako hayabadiliki na kuwa bora kwa namna yoyote ile.

Mifano zaidi, unapotumia vilevi na kujisikia vizuri kilevi kinapokuwa mwilini lakini kikiisha maisha yako ni yale yale. Na hivi unajua kuna baadhi ya watu wanafanya uhalifu fulani kwa kuwa wanataka tu umaarufu? Yote hayo ni katika kutafuta ushindi kwenye usumbufu, ushindi usiokuwa na manufaa.

Ushindi wa kweli, ushindi ambao utakuwa na manufaa kwako ni ushindi wa kujitambua mwenyewe na kuchagua kuyaishi maisha yako. Pambana na huo na achana na ushindi mwingine feki unaotokana na usumbufu mbalimbali.

## Kila mtu hawezi kuwa kama wewe.

Watu wengi wanapata maarifa ya aina hii, wanaooneshwa namna dunia inavyowahadaa na kuwapoteza, hujitetea kwa hoja dhaifu

kwamba lakini lazima dunia iende na kila mtu akiwa hivyo basi dunia haiwezi kwenda.

Kwamba kama kusipokuwa na mashabiki wa mpira wachezaji watawezaje kunufaika na vipaji vyao. Kwamba kama kusipokuwa na walevi, wakulima wanaolima mali ghafi zinazotengeneza vilevi wataishije?

Wengi huona kwa kutokuyaishi maisha yao, wanachangia kwenye kuifanya dunia iende. Lakini hiyo ni hoja dhaifu kwa sababu mbili.

Moja dunia huwa haiendeshwi na mtu yeyote mmoja au kikundi fulani cha watu. Dunia inajiendesha kwa kanuni zake yenyewe na sisi huwa tunajibadilisha ili kuendana na vile dunia inavyokwenda.

Hivyo kama kila mtu ataacha kutumia vilevi leo, wakulima wanaolima mazao yanayozalisha vilevi hivyo watagundua mazao yao hayana tena soko na hapo watalazimika kulima mazao mengine yenye soko. Hivyo ndivyo dunia na hata uchumi unavyojiendesha, kulingana na mahitaji yaliyopo.

Mbili ni kwamba kila mtu hawezi kuwa kama wewe. Kwa sababu hakuna watu wawili wanaofanana kwa kila kitu, kila mtu akijitambua na kuishi maisha yake, tutakuwa na dunia yenye utofauti mkubwa baina ya watu na utofauti huo ndio unaopelekea maisha kuwa bora kabisa.

Kwa sababu watu wanapokuwa tofauti ndiyo wanategemeana zaidi kwa namna ambayo kila mmoja ana mchango kwa mwenzake, hilo linaimarisha ushirikiano na kuthaminiana.

Jamii hiyo itakuwa bora kuliko ya sasa ambayo baadhi ya watu wanaona wako juu ya wengine na kujinufaisha kupitia wale wasiojitambua.

Kama tulivyoona, kama kila mtu akijitambua na kuyaishi maisha yake, magereza yatakosa watu na hata hakutakuwa na uhitaji wa maigizo mbalimbali. Kwa sababu kitu watu wanafuata kwenye kuangalia maigizo, tamthilia au kusoma riwaya, ni kuyaona maisha ambayo wao wameshindwa kuyaishi. Ndiyo maana kila tamthilia au riwaya huwa ina shujaa, kila

msomaji huwa anajiweka sehemu ya shujaa hiyo.

Usihofie kwamba kila mtu akijitambua basi kuna vitu vitakosa soko, jua soko litakuwa bora na pana zaidi kwa vitu vilivyo sahihi.

## Sehemu isiyo na ushindani.

Kila jamii imejengwa kwenye mfumo wa piramidi, chini kunakuwa na mrundikano wa wengi, wakati juu ya piramidi kunakuwa na wachache.

Piramidi ni kama mlima, ambapo chini kuna mkusanyiko wa watu wengi na hivyo hewa inakuwa siyo safi na ya kugombania na wengine, wakati kileleni kuna wachache na hewa ni safi, isiyo ya kugombania.

Kwenye kazi au biashara yoyote unayofanya pia ipo kwa mfumo wa piramidi. Chini wamekusanyika wengi ambao wanafanya kwa mazoea, kama ambavyo wengine wanafanya. Hawa huwa wanakuwa na ushindani mkali kwa sababu hakuna kinachowatofautisha.

Kwenye kilele kunakuwa na wachache ambao wamechagua kufanya tofauti, ambao wameweka utu wao kwenye kile wanachofanya na hivyo kujitofautisha kabisa na wengine. Hawa wanakuwa hawana ushindani kabisa na wanapata manufaa makubwa.

Hivyo kwa chochote unachofanya, nenda eneo lisilo na ushindani na eneo hilo ni kukifanya kama wewe.

Jitambue wewe mwenyewe kwa kuyajibu maswali matatu uliyojifunza hapa, kisha kifanye kitu hicho kulingana na majibu uliyojipa. Kwa kuchagua kufanya hivyo hutamridhisha kila mtu, hivyo lazima uwachague wale sahihi na watakaonufaika zaidi, kisha fanya kitu hicho kwa upekee wa juu sana, upekee ambao haupatikani pengine.

Unapojitambua na kuchagua kuwa wewe, unapofanya kile unachofanya kwa kuweka utu wako, unakuwa kitu ambacho hakijawahi kuwepo duniani na jamii haiwezi kuleta mtu mwingine anayeweza kufanya kama wewe.

Hilo linakuweka kwenye ushindi wa juu kabisa, ushindi ambao hakuna anayeweza kushindana na wewe. Kwa sababu hakuna mwingine kama wewe, jamii italazimika kukupa kile unachotaka ili inufaike na kile ulichonacho. Na hapo ndipo unapoona umuhimu wa kuwa na majibu ya yale maswali matatu, kwa sababu mwisho wa siku siyo tu kukuhusu wewe, bali manufaa unayotoa kwa wengine pia.

Lakini kama ambavyo tumejifunza, unapokuwa juu, kwa kuwa wewe, bado jamii itakuwa inapambana kukuangusha, hivyo hupaswi kujisahau. Kila siku unapaswa kuendelea kupambana kuwa wewe ili uendelee kubaki kwenye kilele cha mafanikio unayokuwa umefikia.

Wale wanaoonja mafanikio na kupotea, wengi wanakuwa walijaribu kuwa wao kwa kipindi kifupi na baadaye wakajisahau na kuacha kuwa wao, jamii ikawaangusha haraka sana.

# Maroboti yatakuacha salama?

Kipindi cha nyuma tulikuwa tunashindana binadamu kwa binadamu, ila sasa tunashindana na maroboti (Artificial Inteligence), ushindani huu ni hatari na utawapoteza kabisa wale wote ambao hawajajitambua na kuyaishi maisha yao.

Tumekuwa na kompyuta kwa muda mrefu, lakini katika kipindi hicho, pamoja na kompyuta kuwa na uwezo mkubwa, zimekuwa haziwezi kufanya maamuzi yake yenyewe, ni mpaka zielekezwe na binadamu.

Lakini teknolojia kwa sasa inakwenda kasi kuzitengenezea kompyuta akili ya kuweza kufanya maamuzi yake yenyewe. Mifano tunaiona kila siku, magari yanayojiendesha yenyewe, vifaa unavyoweza kuongea navyo na vikachukua hatua, mfano programu ya SIRI iliyo kwenye simu za Iphone na kadhalika.

Teknolojia hizi zinakwenda mbali zaidi, sasa kuna kompyuta zinazoweza kufanya operesheni kwa binadamu na kwa mafanikio makubwa. Huku nyingine zikitoa huduma mbalimbali kama

kuwahudumia wateja mgahawani au kupokea na kujibu simu kwenye vitengo vya wateja.

Cha kushangaza ni kwamba, sasa kuna kompyuta zinaweza kuandika makala na hata vitabu, kwa kukusanya maarifa mbalimbali yaliyo mtandaoni na kuja na uandishi ambao mtu wa kawaida hawezi kujua kwamba umefanywa na kompyuta na siyo mtu.

Kama ulifikiri kompyuta zitaendelea kututegemea sisi, ulijidanganya, kompyuta zinakua na zitaanza kujitegemea zenyewe. Lakini pamoja na kompyuta hizo kuweza kujitegemea zenyewe, bado haziwezi kuwa na ile nafsi ambayo mtu anayo, haziwezi kuwa na kusudi ambalo mtu anaweza kuwa nalo.

Ndiyo maana watu pekee watakaoweza kushindana na kompyuta hizi zenye akili, ni wale waliojitambua na kuchagua kuyaishi maisha yao kwa uhalisia na siyo kuiga wengine na kufuata mkumbo.

Wale wote wanaofanya kazi au biashara zao kwa mazoea na kufuata mkumbo, kompyuta

zimeshawapunguza sana na ujio wa kompyuta zenye akili utawaondoa kabisa.

Jitambue wewe mwenyewe, chagua kuwa wewe na hakuna roboti litakaloweza kuchukua nafasi yako kamwe.

## Usirudie makosa kwa watoto.

Huenda wazazi wako walikulazimisha uwe na maisha ya aina fulani, hukupenda lakini ilibidi ukubaliane nao kwa sababu ulikuwa huna namna nyingine. Sasa umekuwa mtu mzima na umeyaona madhara yake, uliwafurahisha wazazi wako, ila wewe huyafurahii maisha yako.

Kwa kawaida, mambo huwa yanajirudia kwenye familia, wengi husema ni laana lakini ukweli ni chochote ambacho mtu alifanyiwa na wazazi wake hujikuta naye akiwafanyia watoto wake.

Hivyo unapaswa kuwa makini usirudie makosa hayo kwa watoto wako, waongoze namna ya kuenesha maisha sahihi na siyo kuwalazimisha wafanye kile unachoona wewe ni sahihi.

Wazazi wengi huwa wana tabia ya kutumia watoto wao kushinda kile ambacho wao walishindwa. Unakuta mzazi alipenda sana kuwa daktari, lakini ikashindikana, hivyo anajipangia lazima mtoto wake awe daktari. Unaweza kumhadaa hivyo mapema, akawa daktari kweli, wewe ukafurahi lakini mtoto asiyafurahie maisha yake yote.

Na pia kuna wale wazazi ambao wanataka watoto wawe na fani kama zao, hawa nao huwahadaa watoto tangu mapema na kujikuta wanaishia kwenye fani za aina hiyo.

Jiepushe sana kufunga wigo wa mtoto akiwa bado ni mdogo. Mwachie uwanja mpana wa kujaribu vitu vingi. Mtu yeyote mwenye miaka chini ya 30 hajajua bado nini anataka hasa kwenye maisha yake. Kwa sababu chini ya miaka 21 hakuna ambaye ameshajitambua kikamilifu. Na baada ya miaka 21 ni wachache sana wanaojitambua kwa ukamilifu. Wengi hutumia miaka ya 20 mpaka 30 na kujaribu vitu mbalimbali mpaka kujua hasa kile wanachokitaka.

Wape watoto wako uhuru huo, waunge mkono kwa kila wanachojaribu, wajifunze na kuona kama wanataka kwenda nacho au la. Usiwalazimishe wala kuwaharakisha, wape muda wa kutosha. Usiwakatishe tamaa kwenye chochote wanachotaka kuwa, bali wasaidie kuuona uhalisia kupitia kujaribu, kisha wajionee wenyewe kama ndiyo kitu wako tayari kukifanya kwa maisha yao yote.

Kwa kufanya hivyo, utaepuka kurudia kwa watoto wako makosa yaliyofanyika kwako na utawaacha wakiwa imara kukabiliana na chochote kuliko hata ukiwaachia mali nyingi huku hawajajitambua. Tunaona kila siku jinsi watoto wanaoachiwa mali nyingi huishia kuzipoteza zote, kwa sababu hawakujitambua kabla hawajaachiwa mali hizo.

Wajibu wako mkubwa kama mzazi ni kumsaidia kila mtoto wako kujitambua na kuyaishi maisha yake, huo ndiyo uridhi bora kabisa unaoweza kuwaachia watoto wako.

Kuwa wewe kwenye dunia hii ambayo inakushawishi kwa kila namna uwe kama wengine, ndiyo ushindi ulio mkuu kabisa kwako. Kuwasaidia watoto wao kuwa wao ni ushindi utakaodumu vizazi na vizazi, kwani nao watawawezesha watoto wao kuwa wao pia. Haya ni mapinduzi ambayo yako ndani ya kila mmoja wetu, tuyafanye kwa kuanza na sisi wenyewe na kwa watoto wetu na wengine wa karibu, bado hatujachelewa, tunaweza kuanza sasa na matokeo yakawa mazuri.

# MAONI, SHUHUDA NA MASWALI.

Karibu kwa maoni, shuhuda na maswali kuhusu barua hii.

Kama kuna mahali hujaelewa na ungependa ufafanuzi zaidi basi karibu uulize swali.

Kama kuna eneo unaweza kuongeza maoni zaidi karibu pia.

Na kama una ushuhuda wa namna umewahi kufanyia kazi yale uliyojifunza kwenye barua hii,

karibu utushirikishe matokeo ambayo uliyapata.

Maoni, maswali na shuhuda viwekwe moja kwa moja kwenye kundi la KISIMA CHA MAARIFA wasap.

Nikutakie kila la kheri katika kufanyia kazi haya uliyojifunza kwenye barua hii.

Rafiki yako anayekupenda sana,

Kocha Dr. Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com/kocha

0755 953 887 / kochamakirita@gmail.com

**MUHIMU;** KAMA HUJAPATA BARUA ZA NYUMA, FUNGUA; www.kisimachamaarifa.co.tz/barua2021